


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO



13 JUNI, 2019

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TANO – TAREHE 13 JUNI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.



Tamko la Sera za Fedha kwa Kipindi cha Mwaka 2018/2019 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2019/2020 (*Monetary Policy Statement for the Year 2019/2020*).

Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Mwaka 2016/2017 – 2018/2019.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

375. MHESHIMIWA MAFTAH ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Vitongoji wanafanya kazi kubwa na ngumu hasa Mtwara Mjini na maeneo mengine ya nchi yetu:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa mishahara kama ilivyo kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa.

376. MHESHIMIWA MARY DEO MURO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Chuo cha FDC kilichopo Shirika la Elimu Kibaha ambacho hakina vifaa vya kujifunzia, karakana zimechoka pamoja na miundombinu mibovu.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO:**

**377. MHESHIMIWA AGNESS MATHEW MARWA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Tangu Ujenzi wa barabara ya Makutano, Sanzati hadi Natta uanze umepita muda mrefu bila Mkandarasi huyo kukamilisha kazi:-

Je, ni lini ujenzi huu utakamilika ili kuwaondolea adha Wananchi wanaotumia barabara hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**378. MHESHIMIWA VEDASTUS MATHAYO
MANYINYI (MUSOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Licha ya kazi nzuri ya waendesha bodaboda ya kurahisisha usafiri na kupunguza tatizo la ajira bado zipo changamoto mbalimbali ambazo ni ajali za mara kwa mara pamoja na wizi:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo hilo;

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutofautisha adhabu ya waendesha bodaboda na ile ya magari makubwa kulingana na vipato vyao.

379. MHESHIMIWA LIVINGSTONE JOSEPH LUSINDE (MTERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo kikubwa cha Polisi katika Jimbo la Mtera hususani katika Kijiji cha Mvumi Misheni ili kukabiliana na wimbi kubwa la uhalifu katika Jimbo la Mtera.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

SAA 10:00 JIONI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020.

DODOMA

S. KAGAIGAI

13 JUNI, 2019

KATIBU WA BUNGE